AckySHINE.com

# Kama wameoana mume na mke na ikatokea hawapati mtoto, je, utajuaje kuwa tatizo liko kwa mwanamke au mwanaume?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kwa wastani i i inachukua kama muda wa mwaka mmoja kwa mwanamke kuanza kupata ujauzito, wakikutana kimwili mwanaume na mwanamke bila kutumia njia ya kupanga uzazi. Wengine wanachukua muda mwingi zaidi, na wengine muda mfupi zaidi. Kama baada ya muda wa mwaka mmoja au mwaka moja na nusu, mwanamke hajashika mimba, watu wanaanza kushangaa na kujiuliza chanzo cha hali hii ni kipi. Kwa sababu kuna vyanzo mbalimbali, lazima mwanaume na mwanamke waende kumwona daktari i i ili wakafanyiwe uchunguzi wa kitaalamu. Halafu daktari anaweza kutambua kama tatizo liko kwa mwanamke au mwanaume au kwa wote wawili. Yaani, bila kumwona daktari haiwezekani kuwa na uhakika tatizo liko kwa nani. Mara chanzo cha tatizo kikijulikana, daktari anaweza kuwashauri mwanamke na mwanaume kuhusu uwezekano wa kuwatibu na kuwasaidia kupata mimba.